Toleo 66 - Dhul Hijjah 1443 AH / Julai 2022 M

# Jarida la UQAB

**TAARIFA KWA VYOMBO VYYA HARABI**
Onyo la Njaa Kubwa Barani Afrika na Uingizaji Siasa Mateso ya Wanawake na Watoto

**HABARI NA MAONI**
Rais Mpya: Hali Imebakia Kama Ilivyokuwa nchini Somalia

**MATOLEO**
Kusimamisha Sheria ya Mwenyezi Mungu Duniani

**JIBU LA SWALI**
Amerika na Mabadiliko katika Mawakala wake nchini Pakistan



Afisi kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا ۚ يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا ۚ وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

حزب التحرير
HIZB UT TAHRIR

KUMB: 37/1443 Alhamisi, 17 Dhul-Qa'adah 1443 H 16/06/2022 M


**Taarifa kwa Vyombo Vya Habari**

# Onyo la Njaa Kubwa Barani Afrika na Uingizaji Siasa Mateso ya Wanawake na Watoto

Rais wa Muungano wa Afrika, Rais wa Senegal Macky Sall alisema katika taarifa kwa Radio France International kwamba Afrika itakabiliwa na njaa mbaya sana, ikiwa usafirishaji wa ngano kutoka Ukraine hadi barani hautaregelewa. Sall alisema, wakati wa taarifa zake kwamba njaa "inaweza kuyumbisha bara." Akizungumzia mkutano wake wa wiki iliyopita na Rais wa Urusi Putin jijini Moscow, alisema alimwomba Putin kuisaidia Afrika kupata mbolea na nafaka. Matamshi haya yalitanguliwa na kauli kadhaa za wanasiasa wa nchi za Magharibi wakihusisha vita vya Ukraine na msukosuko wa chakula barani humo, hasa kauli za Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Fedha wa Kimataifa (IMF) kwamba "kusema kwa ufupi, vita barani Ulaya, Ukraine, vinatafsiriwa kuwa njaa barani Afrika," na kauli ya rais wa Ufaransa, "Tunatarajia njaa barani Afrika kwa sababu ya vita vya Urusi dhidi ya Ukraine." Kauli hizi, kwa ujumla wake, hazikuwa chochote ila chombo cha propaganda kati ya Urusi na Magharibi. Urusi ilikutana na taarifa hizi za kushangaza za nchi za Magharibi kwa shutma za moja kwa moja kwamba vikwazo vya Magharibi vilizidisha janga la chakula na kufunga maduka ya nafaka na mbolea.

Wakati wanasiasa wakilaumiana wao kwa wao kwa kupatiliza mateso ya binadamu kama silaha ya vita, taswira ya miili ya Waafrika iliyodhoofika na kina mama walio na huzuni imeregea katika vichwa vya habari, kama vile matukio ya watoto wenye utapiamlo katika pwani ya Afrika au Afrika Mashariki, kana kwamba picha ilikuwa haijabadilika na wakati ulikuwa umesimama katika mandhari ile ile ya kusikitisha miongo kadhaa iliyopita. Nyuso ni zile zile, na ulimwengu unasimama bila hatua yoyote mbele ya kambi za njaa na msaada zinazotarajiwa ambazo wengine huzifikia baada ya safari ndefu kwa miguu, huku wakizika watoto na wazee wao waliokufa. Hii inafanywa ndani ya muundo wa uangaziaji wa vyombo vya habari ambao unaingizwa siasa katika umbo na maudhui na hauna uhusiano wowote na wanadamu. Licha ya uzito wa hali hiyo na taarifa nyingi zinazosikika, kuna upungufu mkubwa wa ufadhili wa mpango wa dharura wa Umoja wa Mataifa kwa nchi zilizoathirika. Taarifa ya pamoja ya mashirika ya Umoja wa Mataifa (WFP, FAO, na UNICEF) ilisema kwamba "asilimia 18 tu ya mpango wa Umoja wa Mataifa wa kukabiliana na hali ya kibinadamu nchini Somalia kwa mwaka 2022 ndio umefadhiliwa."

Mbali na milipuko ya kisiasa, Oxfam na Save the Children wameielezea hali ya Afrika Mashariki kuwa ni ya janga, na kubainisha kuwa mtu mmoja hufariki kwa njaa kila baada ya sekunde 48, na njaa hiyo inadhihirisha kufeli mara kwa mara kwa duniani kuepusha majanga yanayoweza kuzuilika.

Tunasimama tena mbele ya uhalisia mchungu ambapo watu wa Bara lenye rutuba la Afrika, tajiri kwa maliasili yake na hali ya hewa ya hali ya juu, hawawezi kupata riziki yao ya kila siku, na kadhia zao nyeti zinatumiwa katika mikataba duni, na wanalipa thamani ya vita vya kirasilimali ambavyo hawana mkono ndani yake.

Suala la usalama wa chakula barani Afrika na kwingineko halitengani na kufikia usalama kwa watu, na haliwezi kuachwa mikononi mwa nchi nyingine, zikilitishia wakati mmoja na kujadiliana nalo wakati mwingine. Wala isiachwe mikononi mwa mashirika ya kimataifa ambayo yanahesabiwa kuwa sehemu kuu ya tatizo, kwani yamefuata sera zilizoharibu uchumi wa nchi na kuweka utiifu na utegemezi kwa wengine. Hizi ni sera zinazowataka wananchi kutumia na kuagiza bidhaa kutoka nje badala ya kuzalisha na kufufua ardhi na kuelekeza kilimo ovyo ovyo katika kutafuta faida ya haraka hivyo kuuchosha udongo bila mafanikio yoyote. Chanzo cha ugonjwa huu sio bei ya juu na ngano ya Urusi wa Ukraine, lakini ni sera hizo zenye kupuuza ardhi na mazao ya ndani, kuzinasibisha riziki za watu na maeneo ya ng'ambo, kuzalisha mazao maalum na kuwalazimisha watu kuagiza ngano kutoka nje, huku tukipuuza kilimo cha kienyeji.

***Endelea... UK 3***


**Email: info@uqab.or.ke**

Kwa miongo kadhaa, Afrika imekuwa ikikabiliwa na umaskini wa fikra, akili na utashi wa kisiasa. Ardhi yake imedhulumiwa kinyama, na watu wake wanakufa kikatili kwa njaa. Afrika haina njia ya kutoka isipokuwa kwa kuifurusha Magharibi na mashirika yake yaliyoifukarisha nchi na kuanzisha majanga matatu, umasikini, ujinga na maradhi. Na haina njia ya kutokea isipokuwa ikiwa watu wake watalima ardhi yao yenye rutuba na kula kile inachokiotesha na kuachana na masuluhisho hadaifu yatokayo nje yaliyoifukarisha nchi na watu. Lakini haiwezekani kwa hili kutokea, isipokuwa kwa kukabiliana na mgogoro wa utawala na kutambua uhalisia wa ukhalifa ardhini.

أَمَّن يُجِيبُ الْمُضْطَرَّ إِذَا دَعَاهُ وَيَكْشِفُ السُّوءَ وَيَجْعَلُكُمْ خُلَفَاءَ الْأَرْضِ أَإِلَـٰهٌ مَّعَ اللَّـهِ قَلِيلاً مَّا تَذَكَّرُون

**“Au nani yule anaye mjibu mwenye shida pale anapo mwomba, na akaiondoa dhiki, na akakufanyeni warithi wa ardhi? Je! Yupo mungu pamoja na Mwenyezi Mungu? Ni machache mnayo yazingatia.” [An-Naml: 62]**

**Kitengo cha Wanawake**
**katika Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**


Email: info@uqab.or.ke

# HABARI NA MAONI
## Rais Mpya: Hali Imebakia Kama Ilivyokuwa nchini Somalia

**Habari:**

Rais wa Somalia Hassan Sheikh Mohamud mnamo Alhamisi alichukuwa uongozi kwa mara ya pili, akiahidi kuyaunganisha makundi yaliyogawanyika nchini mwake, pamoja na kuleta uhusiano mwema na majirani zake baada ya miaka mingi ya mizozo. Mohamud, alipochukua uongozi kutoka kwa Mohamed Farmaajo, alisema kuwa nchi yake itachukua msimamo wa kati na kati katika masuala ya kimataifa, huku ikijikurubisha kwa nchi zinazo heshimu ubwana wake na kutafuta suluhisho kwa matatizo ya pamoja kama al-Shabaab na umasikini. “Tukio tunaloshuhudia leo [kutawazwa kwake] ni mfano wa kukita kwa demokrasia katika taasisi nchini Somalia,” alisema, alisisitiza kwamba isipokuwa pale ambapo nchi ilikuwa chini ya utawala wa kijeshi kwa miaka 21 (1969 – 1991), Wasomali wamekuwa wakiegemea demokrasia. (The EastAfrican, Ijumaa, 10 Juni 2022).

**Maoni:**

Vyombo vya habari nchini, kieneo na kimataifa vimepongeza uhamishaji wa mamlaka kwa amani kutoka utawala wa zamani hadi mpya. Kiujanja, vimefeli kutaja kwamba rais mpya haleti lolote jipya kuhusiana na sera wala sheria kando na kumakinisha hali iliyoko sasa inayoikumba Somalia. Mwanzoni, alikuwa uongozini kutoka mwaka 2012 – 2017 kipindi ambacho Somalia ilishuhudia mtafaruku mkubwa wa kisiasa, kiuchumi na kijamii na ambao unaendelea hadi sasa. Rais mpya anaingia uongozini kwa mara ya pili, akiwa mwingi wa ahadi lakini ni porojo tupu.

Somalia inakumbwa na matatizo mengi ambayo yanahitaji utatuzi wa kweli na dharura. Baadhi ya matatizo yanajumuisha ukame wa kujirudia ambao unaendelea kuwadhikisha watu. Uporaji wa kupindukia wa rasilimali za umma kupitia kampuni za kigeni ambazo zinafanya miamala ya kisiri na walioko mamlakani. Ufadhili na uchocheaji wa kimakusudi wa makundi ya kisilaha na mizozo ya kikabila kupitia mikono ya wageni ambao hunufaika kwa ukosefu wa usalama endelevu nchini Somalia ni tatizo jingine kubwa.

Utawala mpya HAUWEZI kattu kusuluhisha changamoto hizo hapo juu, kwa sababu msingi wa utawala wenyewe unahitaji kubadilishwa. Hakika, hali imebakia kama ilivyokuwa nchini Somalia kwa kuwa utawala mpya ni muendelezo wa nidhamu ya sumu iliyopo na ambayo msingi wake ni mfumo wa kisekula wa kirasilimali. Nidhamu ya utawala ambayo imeiweka mbali dini kuhusiana na masuala ya utungaji sheria! Hivyo basi, imeipa kipaumbele akili ya mwanadamu yenye kikomo katika kusimamia mambo ya watu kwa kutegemea kubahatisha waliko kuchukua kutoka kwa mabwana zao wakoloni Wamagharibi.

Kwa hiyo, watu nchini Somalia wameruka kutoka katika kikaango kimoja kwenda kingine, kwa kuwa suala la dharura zaidi linalohitaji utatuzi ni kubadilisha nidhamu ya uongozi ya kisekula ya kidemokrasia ambayo inatanua kupitia fujo na uchafu. Badala yake kuweka katika sehemu yake nidhamu ya utawala ya Kiislamu ya Khilafah, nidhamu inayochipuza kutoka kwa Muumba wa ulimwengu, mwanadamu na uhai kwa maana Mwenyezi Mungu (swt). Khilafah hainasibishwi na wakoloni Wamagharibi ambao wanaushawishi katika sera ya ndani na nje kama inavyofanyika nchini Somalia na kwingineko duniani. Kwa mfano, uchaguzi wa hivi juzi wa urais ulifanyika mnamo Mei 2022 kama natija ya msukumo ili kutimiza masharti ya kigeni yaliyowekwa na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) ili kuiwezesha Somalia kupata kitita cha dola milioni 400 kama msaada ikiwemo ahadi nyingine za kutoka ng’ambo! (Reuters, 16 Mei 2022).

Hivi sasa Somalia inataabika kutokamana na kukosekana uongozi wa Kiislamu. Wale walioko mamlakani sio chochote bali ni watawala vibaraka wa wakoloni Wamagharibi. Kuwepo kwao madarakani ni kwa ajili ya kulinda maslahi ya mabwana zao na kutekeleza sera wanazochorewa kutoka katika miji mikuu ya Wamagahribi hususan Washington na London. Muonekano wao kiinje na wawenzao kutoka Mashariki ya Kati na ulimwengu wa Waislamu kwa ujumla huwahadaa watu kwamba wao ni ngao na walinzi wa kweli wa Waislamu na Uislamu. Alas, sio wa kweli, kwa kuwa hawana utambulisho wa Kiislamu kwa maana wanavyofikiria na kutenda ni kinyume na maamrisho ya Uislamu kama ilivyoletwa na Mtume (saw).

Kinyume chake, Khilafah itaongozwa na mwanamume Muislamu, Khalifah ambaye atajituma usiku na mchana kutekeleza nidhamu za Kiislamu zinazochipuza kutoka kwa Shari’ah ya Kiislamu ambayo inadhamini utulivu na ustawi kwa wote pasi na kuzingatia rangi, kabila wala dini. Pia, atakuwa ndiye mlinzi na ngao kwa walioko chini yake na hususan heshima ya Mtume (saw) ambayo inakejeliwa hadi leo na maadui wa Uislamu na Waislamu. Hali ya kusikitisha ya Somalia itadumu, mpaka pale ambapo Waislamu wa kweli ndani na nje watatambua makosa ya kimsingi ya kubeba mfumo wa kisekula wa kirasilimali, na kuanza kufanyakazi na Hizb ut Tahrir ili kurudisha tena maisha ya Kiislamu kwa kusimamisha Khilafah kwa njia ya Utume. Wakati ni sasa, upatilize na hautojuta.

**Imeandikwa kwa ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Ali Nassoro Ali**
**Mwanachama wa Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

# Kusimamisha Sheria ya Mwenyezi Mungu Duniani Ni Ahadi ya Uongozi wa Kweli ambayo Hujadidishwa Hadi Mwenyezi Mungu Akamilishe Miadi Yake





**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na
Zeina As-Samit**


Utukufu ni Wake ambaye amemuumba mwanaadamu na kumtengeneza, akampulizia roho, na akamtunukia akili. Utukufu ni Wake ambaye amempeleka Mjumbe Wake kuwa ni rehma kwa walimwengu na kuwatoa katika giza la ukafiri kwenda kwenye mwangaza wa imani. Utukufu ni Wake, ambaye ameteremsha Kitabu Chake kwa Mtume Wake, Aliyemchagua, kuwa ni alama na taa yenye kuangaza njia kwa watu wote. Utukufu ni Wake ambaye amesema:

وَمَا خَلَقْتُ الْجِنَّ وَالْإِنْسَ إِلَّا لِيَعْبُدُونِ * مَا أُرِيدُ مِنْهُم مِّن رِّزْقٍ وَمَا أُرِيدُ أَن يُطْعِمُونِ

**“Nami sikuwaumba majini na watu ila waniabudu mimi. Na sitaki kwao riziki wala sitaki wanilishe.”** [Adh-Dhariyat: 56-57]. Utukufu ni Wake ambaye amesema:

قُلْ إِنَّ صَلاَتِي وَنُسُكِي وَمَحْيَايَ وَمَمَاتِي لِلّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ * لاَ شَرِيكَ لَهُ وَبِذَلِكَ أُمِرْتُ وَأَنَاْ أَوَّلُ الْمُسْلِمِينَ.

**“Sema : Hakika Swala yangu, na ibada zangu, na uhai wangu, na kufa kwangu, ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa viumbe vyote. Hana mshirika wake. Na hayo ndiyo niliyoamrishwa, na mimi ni wa kwanza wa Waislamu.”** [Al-An'am: 162-163].

Mwenyezi Mungu ameumba waja Wake na kuchukua ahadi kwamba watashuhudia kuwa Yeye ndio Mola wao

وَإِذْ أَخَذَ رَبُّكَ مِن بَنِي آدَمَ مِن ظُهُورِهِمْ ذُرِّيَّتَهُمْ وَأَشْهَدَهُمْ عَلَى أَنفُسِهِمْ أَلَسْتُ بِرَبِّكُمْ قَالُوا بَلَى شَهِدْنَا أَن تَقُولُوا يَوْمَ الْقِيَامَةِ إِنَّا كُنَّا عَنْ هَذَا غَافِلِينَ

**“Na pale Mola wako Mlezi alipowaleta katika wanaadamu kutoka migongoni mwao kizazi chao, na akawashuhudisha juu ya nafsi zao, akawaambia: Je, Mimi si Mola Mlezi wenu? Wakasema: Kwani! Tumeshuhudia. Msije mkasema Siku ya Kiyama sisi tulikuwa tumeghafilika na hayo.”** [Al-A’raf: 172].

Ameleta sheria zake ili wale walioko duniani waweze kuishi maisha bora, wakihakikishiwa kwa hukumu zake kuwa hawatoingia kwenye batili au kwenye dosari, zitakazosimamishwa miongoni mwao na kiongozi mcha Mungu. Mwenyezi Mungu (swt) ameuchagua Ummah wa Mtume Wake (saw) kuwa ummah bora ulioletwa kwa watu wanaolingania mema, kuamrisha mema na kukataza maovu, kuwa ni Ummah ambao unaongoza ummah nyengine kwa kile kinachomridhisha Yeye, Utukufu ni Wake

كُنتُمْ خَيْرَ أُمَّةٍ أُخْرِجَتْ لِلنَّاسِ تَأْمُرُونَ بِالْمَعْرُوفِ وَتَنْهَوْنَ عَنِ الْمُنكَرِ وَتُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَلَوْ آمَنَ أَهْلُ الْكِتَابِ لَكَانَ خَيْراً لَّهُم مِّنْهُمُ الْمُؤْمِنُونَ وَأَكْثَرُهُمُ الْفَاسِقُونَ

**“Nyinyi mmekuwa bora ya umma waliotolewa kwa watu, kwa kuwa mnaamrisha mema na mnakataza maovu, na mnamuamini Mwenyezi Mungu. Na lau kuwa watu wa Kitabu nao wameamini ingelikuwa bora kwao. Wapo miongoni mwao waumini, lakini wengi wao wapotovu.”** [Aali-’Imran :110].

Moja ya Sunnah Zake, Aliyetukuka, ni kuwa amefanya uongozi kuwa ni hitajio la maisha kuendesha mambo ya viumbe Vyake, hivyo makundi ya ndege wana kiongozi

***Endelea... UK 6***

anayewaongoza, na ng'ombe na wanyama wanaye anayewaongoza, pamoja na wadudu na nyuki… Wote ni umma kama wanaadamu

وَمَا مِنْ دَابَّةٍ فِي الأَرْضِ وَلا طَائِرٍ يَطِيرُ بِجَنَاحَيْهِ إِلَّا أُمَمٌ أَمْثَالُكُمْ مَا فَرَّطْنَا فِي الْكِتَابِ مِنْ شَيْءٍ ثُمَّ إِلَى رَبِّهِمْ يُحْشَرُونَ

**"Na hapana mnayama katika ardhi, wala ndege anayeruka kwa mbawa zake mbili, ila ni umma kama nyinyi. Hatukupuuza Kitabuni kitu chochote. Kisha kwa Mola wao Mlezi watakusanywa."** [Al-An'am:38].

Uongozi ni mamlaka ya kuwaongoza na kuendesha maisha, na ni suala la msingi kwa utekelezaji wake. Na Mwenyezi Mungu Mtukufu ameiweka bay'ah kwa kiongozi Ummah wa Kiislamu ili kutekeleza hukmu za Mwenyezi Mungu na Amewajibisha kwa Ummah kumtii Yeye isipokuwa akiwaamrisha kuasi hapo hatosikilizwa wala kutiiwa.

Mtume (saw) alikuwa kiongozi wa mwanzo wa Ummah wa Kiislamu na ni mtu mtukufu zaidi anayejulikana kwa wanaadamu; amefikisha ujumbe, ametimiza amana, na ameuwacha Ummah wa Kiislamu ukiwa mtukufu na wenye nguvu, ulioongoza mataifa na kueneza mwanga na uongofu wa Mwenyezi Mungu, na wanaadamu hawajashuhudia kiongozi mtukufu zaidi kuliko yeye; Yeye ndiye aliyewaleta watu pamoja wakiwa katika makabila na asili, makundi na rangi tofauti chini ya bendera ya "Laa ilaaha illallah", akivunja mipaka na kuunganisha nyonyo.

Kumuabudu Mwenyezi Mungu maana yake ni kuijaza watu ardhi na kueneza hikma Zake juu yake. Yaani amana ambayo mbingu, ardhi, na milima ilikataa kuibeba na ambayo mwanaadamu aliichukua. Mitume na Manabii waliipokea, na Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) alikuwa ni wa mwisho wao kuitekeleza amana hii kubwa kwa kiwango cha hali ya juu kabisa na kumridhisha Mola wake na akimshuhudia kuiweka amana hii kwa Ummah wake kuendelea kutembea juu ya njia yake na kufuata njia yake katika kutekeleza ahadi alizoziweka kuihifadhi dini ya Mwenyezi Mungu na kuieneza duniani kote.

Ilikuwa ni ahadi ya kiongozi mkweli, muadilifu, muaminifu, asiye na jengine ila kumridhisha Mola wake na kueneza sheria zake kwa watu wote ili maisha yawe kama Mwenyezi Mungu anavyopenda na kuridhika nayo kwa waja Wake.

فَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّن كَذَبَ عَلَى اللَّهِ وَكَذَّبَ بِالصِّدْقِ إِذْ جَاءَهُ أَلَيْسَ فِي جَهَنَّمَ مَثْوًى لِّلْكَافِرِينَ * وَالَّذِي جَاءَ بِالصِّدْقِ وَصَدَّقَ بِهِ أُولَئِكَ هُمُ الْمُتَّقُونَ * لَهُم مَّا يَشَاءُونَ عِندَ رَبِّهِمْ ذَلِكَ جَزَاءُ الْمُحْسِنِينَ

**"Basi ni nani dhalimu mkubwa kuliko yule aliye msingizia uwongo Mwenyezi Mungu na kuikanusha kweli imfikiapo? Je! Sio katika Jahannamu makaazi ya hao makafiri? Na aliyeileta kweli na akaithibitisha – hao ndio wacha mungu. Watapata watakacho taka kwa Mola wao Mlezi. Hayo ndiyo malipo ya watendao mema".** [Az-Zumar: 32-34]

Na juu ya njia yake, masahaba zake walitembea, na walikuwa kwenye kile alichowawekea na kile alichowafundisha katika kuihifadhi dini na kufanya kazi kuieneza, kutekeleza maslahi ya Ummah, kueneza uadilifu na amani, na kujitahidi kutosheleza mahitaji ya kila mtu anayehusiana na serikali ya Kiislamu na katika kuhudumia dini na kusimamisha neno lake, wanatumia fedha zao, na kwa ajili ya maisha ya baadaye na kwa ajili ya radhi za Mwenyezi Mungu wanatumia kile walichonacho. Wanafanyakazi katika kuimarisha utekelezaji wa hukumu zake juu ya waja, kuwahofisha kwa Mwenyezi Mungu na juu ya ghadhabu Zake kama watakuwa na upungufu au kutenda makosa. Wanahudumia raia zao na kuwapatia mahitaji yao, hasa vikongwe, na wale wasio na wasimamizi. Na habari ya bibi kipofu aliyehudumiwa na Abu Bakar, Khalifah wa Mtume wa Mwenyezi Mungu, na baadaye kuendelea kuhudumiwa na Omar Ibn Al-Khattab (ra), ni mfano mwema wa mashindano kwa huduma bora na raha ya mmoja wao kwa ajili ya mwengine kwa hilo ni "Wewe umewamaliza Makhalifah baada yako, Ewe Abu Bakar…" Wamechukua nafasi ya uongozi baina yao, na kila mmoja kati yao akijibidiisha kuitekeleza kwa wema katika namna ambayo itamridhisha Mwenyezi Mungu. Na wakimhofu Mwenyezi Mungu hata kwa ajili ya ndege (wakieneza mapenzi kwao ili wasikae na njaa) na wanyama (wakiwasawazishia njia ili wasijikwae)!

Uaminifu ulitekelezwa na Makhalifah wa Waislamu, kila mmoja kwa kadiri ya uchamungu wake na hofu kwa Mwenyezi Mungu (swt). Wamejitahidi kuihifadhi dini hii na kuilinda na kuieneza katika maeneo yote ya dunia ili neno la Mwenyezi Mungu liwe juu na hukumu ziwe kwa Mwenyezi Mungu Mmoja tu, lakini maadui wa dini hii na kwa msaada wa kikundi kidogo cha vijana wa Ummah waliomkhini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake na kupuuza amana na kuiuza, waliweza kuiangusha dola ya Khilafah. Umbo la kisiasa linaloihifadhi dini na ambalo linaegemea juu ya utekelezaji wa sheria zake, wameligawanya katika vijidola tofauti tofauti na wakaweka humo mawakala wao, kwa msingi wa maslahi yao na kuwahifadhia uporaji wa utajiri na ardhi ya Ummah. Mambo yalipewa wale wasiostahiki, na mambo yanapopewa yule asiyestahiki basi tusubiri kuja kwa kiyama kama Mtume (saw) alivyotuambia: «إِذَا ضُيِّعَتْ الْأَمَانَةُ فَانْتَظِرْ السَّاعَةَ» قَالَ: كَيْفَ إِضَاعَتُهَا يَا رَسُولَ اللَّهِ؟ قَالَ: «إِذَا أُسْنِدَ الْأَمْرُ إِلَى غَيْرِ أَهْلِهِ فَانْتَظِرْ السَّاعَةَ» "Amana itakapopotea basi isubiri Saa ya Kiyama" Pakaulizwa, "Vipi kupotea kwake, ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu?" Akasema, "Watakapopewa mamlaka wale wasiostahiki, basi isubiri Saa ya Kiyama" [Imepokewa na Al-Bukhari].

Mambo yanawachiwa wale wasioshughulika na kuwahudumia watu na hawasimamii maslahi yao. Wanawabebesha mizigo ya kodi na bei kubwa, na wanawanyima utajiri ambao Mwenyezi Mungu

*Endelea... UK 7*

 Email: info@uqab.or.ke

amewapatia. Mambo yameachiwa wale wanaouza nchi na kueneza dhulma miongoni mwa watu na kueneza uchafu na ufisadi miongoni mwao.

Basi wako wapi wale wanaosimamia maslahi ya watu na kuwatawala kwa mfumo wa kibinadamu unaojali maslahi ya wachache na kuwakandamiza walio wengi ambapo watoto wanataabika duniani (vita, ukame, unyanyasaji wa kimwili na wa kijinsia)?! Wako wapi na hofu wanayoishi nayo na kuhamahama kwa watu hawa, hasa watoto wa Waislamu?! Wako wapi wale wanaotawala kwa mfumo usioweza kutoa huduma na ambao hauwapatii mahitaji ya kibinadamu ambapo maelfu ya watoto wanafariki kwa njaa au wanaoponea kwa majani na mabaki ya vyakula ili kupitisha siku?! Na ilhali ni watoto wa Ummah walio na utajiri, basi ni kipi kinacho wadhaminia maisha bora?!

Kuna tafauti kubwa baina ya watu hawa na wale wanaohukumu kwa sheria za Mwenyezi Mungu, wanahuruma kwa watoto na kuwaheshimu wazee! «لَيْسَ مِنَّا مَنْ لَمْ يَرْحَمْ صَغِيرَنَا وَيُوَقِّرْ كَبِيرَنَا» **“Sio katika sisi yule asiyewarehemu wadogo wetu na kuwaheshimu wakubwa wetu”** [Imepokewa na Abu Dawud na Tirmidhi]

Kuna tafauti baina yao na wale wanaopangusa vichwa vya mayatima na kuwapatia yale wanayoyahitaji!

Wako wapi watawala leo wakati kuna wanaotaabika kutokana na umasikini na kukosa ajira?! Wako wapi vijana wa Ummah wanaomaliza maisha yao kwa kujinyonga, kuzama, au kuungua wakati milango yote imefungwa machoni mwao, na maisha yao yamekuwa ya kiza na ya kukata tamaa, na kuchanganyikiwa kumekuwa ndio kitambulisho chao?!

Wako wapi na maumivu ya vijana wetu wakati wakiwa wamezungukwa na mto wenye nguvu wa mitihani na majaribu?! Wanaishi maisha yanayowavuta kwenye makatazo yote na yanayowakataza usafi na utakaso wa kijinsia! Wako wapi waliochukua amana na kujitahidi kuihifadhi na kumhofu Mwenyezi Mungu katika ujana, ili wawasaidie kufunga ndoa, kuwasamehe na kuwasaidia kutosheleza matashi yao kwa mujibu wa sheria ambazo Mwenyezi Mungu (swt) ameziagiza na kuziridhia?! Kutoka kwa Abu Huraira (ra) amesema, Mtume wa Mwenyezi Mungu (swt) amesema, «ثَلَاثَةٌ حَقٌّ عَلَى اللَّهِ عَوْنُهُمْ؛ الْمُجَاهِدُ فِي سَبِيلِ اللَّهِ، وَالْمُكَاتَبُ الَّذِي يُرِيدُ الْأَدَاءَ، وَالنَّاكِحُ الَّذِي يُرِيدُ الْعَفَافَ» **Watu namna tatu Mwenyezi Mungu ana haki ya kuwasaidia: Anayepigana Jihad katika njia ya Mwenyezi Mungu, na mtumwa anayetaka kujikomboa, na anayeoa ambaye anataka maisha ya kujitakasa kutokana na uchafu.”**

Wako wapi watawala hivi leo wakati vijana hawawezi kujikimu gharama za ndoa au kusaidia familia na kutosheleza gharama (ukosefu wa kazi umeenea na gharama za ndoa na maisha ni kubwa mno…)?!

Wako wapi watawala, wakati mwanamke anaponyanyaswa, kukandamizwa, kutiwa utumwani, kudanganywa kwa kauli za uhuru na haki wakati yuko katika minyororo, akisubiri wakumuacha huru kutoka kwenye maisha haya ya taabu yanayomfanya apoteze ujanajike wake ambao Mwenyezi Mungu amemuumba nao?!

Wako wapi wale wanaodai kuongoza ulimwengu kutokana na ukame, umasikini, ukosefu wa kazi na vita ambapo dunia yote imeathirika navyo?! Kutoka kwenye maisha ya ovyo, vifua vya watu vimebinywa na shingo zao zimebanwa, wakisubiri mfumo mwengine unaojali maslahi ya watu wote: masikini na tajiri, wadogo na wakubwa, wanaume wao na wanawake wao, unaomhudumia mwanaadamu kama mwanaadamu?!

Je, ana mfumo bora zaidi kuliko ule wa Muumba kushughulikia maslahi yake na kutosheleza mahitaji yake?

أَلاَ لَهُ الْخَلْقُ وَالأَمْرُ تَبَارَكَ اللّهُ رَبُّ الْعَالَمِينَ

**“Fahamuni! Kuumba na amri ni zake. Ametukuka kabisa Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa viumbe vyote!”** [Al-A’raf: 54]

Wao wako wapi na wapi na viongozi wakweli wenye ufahamu juu ya amana ambayo Mwenyezi Mungu amewakabidhisha kwa waja Wake na kuwa imebebwa na viumbe bora zaidi, masahaba zake, na kila ambaye ni mkweli kwa Mwenyezi Mungu? Yeyote aliye mkweli na akawa anatekeleza amana ataokoka, na anayekosa na kudanganya amekhini na atajuta siku ambayo majuto hayatamfaa!

Uongozi wa kweli unabeba wito wa Mwenyezi Mungu na unakumbusha ukweli pamoja na Mwenyezi Mungu, unabeba ushughulikiaji wa ujumbe huu na ushughulikiaji wa dini hii na unafanyakazi kuihifadhi na kuitukuza juu ya ardhi, bila kujali lawama ya mwenye kulaumu na sio wenye kuvunjwa moyo na wachache wanaofuata njia hii. Ni ule unaofanya kazi kuongoza sheria za Mwenyezi Mungu na kujengwa juu ya kumfanya atawale ardhi kwa nguvu zote na mshikamano. Hana maridhiano (na maadui wa Uislamu), hana kijalizo (juu ya mambo ya dini), havumilii (juu ya ukiukaji sheria). Una ushupavu wa kushinda wasiwasi wote, na uimara na ushujaa, unakataa kila uzembe au kurudi nyuma. Ni uaminifu na unyenyekevu wake kwa Mwenyezi Mungu, Msaidizi, Mtoaji ushindi, Mwenye nguvu zaidi.

Uongozi wa kweli ni jukumu, na kila anayemhofu Mwenyezi Mungu hahofii kuutendea haki yake في رواية عن أبي ذرّ قال: قلت يا رسول الله، ألا تستعملني؟ فضرب بيده على منكبي ثم قال: «يَا أَبَا ذَرٍّ إِنَّكَ ضَعِيفٌ، وَإِنَّهَا أَمَانَةٌ، وَإِنَّهَا يَوْمَ الْقِيَامَةِ خِزْيٌ وَنَدَامَةٌ، إِلَّا مَنْ أَخَذَهَا بِحَقِّهَا، وَأَدَّى الَّذِي عَلَيْهِ فِيهَا» **“Kutoka kwa Abu Dharr alimwambia Mtume (saw): Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, hunipatii uongozi (ugavana)? Mtume (saw) akampigapiga begani kisha akamwambia: “Ewe Abu**

*Endelea... UK 8*


Email: info@uqab.or.ke

**Dharr, wewe ni dhaifu, na huu uongozi ni amana, nao siku ya kiyama itakuwa ni sababu ya hizaya na majuto, isipokuwa kwa yule atakayeuchukua kwa haki yake na kuutekelezea humo wajibu wake." Katika mapokezi mengine alimwambia, "Ninakuona wewe ni dhaifu Abu Dharr, na ninakutakia kile ninachojitakia mimi. Usikubali utawala juu ya watu wawili na usiwe msimamizi wa mali ya mayatima."** [Imepokewa na Muslim]

Uongozi wa kweli ni ule ambao mazingatio yake yamejengwa juu ya utekelezaji wa hukumu za Mwenyezi Mungu juu ya watu kuangazia maisha yao pamoja nao, ili ukamilifu wa Sharia za Mwenyezi Mungu udhihiri katika kutatua matatizo yao, kuhifadhiwa mahitaji yao na kuhakikishiwa maisha bora. Kueneza haki na wema miongoni mwao na kuwafanya wajihisi salama na wataingia kwenye Uislamu kwa makundi. Kiongozi mkweli ni yule asiyeiona dunia isipokuwa ikitawaliwa, ikimilikiwa, na kuongozwa kwa sheria za Mwenyezi Mungu kwa sababu anauhakika wa ahadi ya Mwenyezi Mungu ya tamkini na ushindi kwa waja Wake waaminifu.

Kiongozi mkweli ni yule anayeweka uaminifu mkubwa juu ya mazingatio yote, kama bwana wetu Abu Bakar, Mwenyezi Mungu awe radhi naye, aliye chukua kutoka mbora wa viumbe na akasuhubiana naye katika hijra. **فَمَنْ كَانَ مِنْكُمْ يَعْبُدُ مُحَمَّداً ﷺ فَإِنَّ مُحَمَّداً ﷺ قَدْ مَاتَ، وَمَنْ كَانَ يَعْبُدُ". اللَّهَ فَإِنَّ اللَّهَ حَيٌّ لَا يَمُوتُ"" "Yeyote kati yenu aliyekuwa akimuabudu Muhammad, basi Muhammad amekufa. Na yeyote aliyekua akimuabudu Mwenyezi Mungu basi Mwenyezi Mungu yuhai na hafi."**

Na katika hatua ya maamuzi, ikaweza kuunganisha umoja wa dola na kuondoa uasi.

Kiongozi mkweli ni yule asiyewadanganya watu wake, ni muaminifu kwa Mwenyezi Mungu na Mtume Wake na Waumini, hufanya kazi mchana na usiku kuregesha utukufu na heshima ya Uislamu na kuwaunganisha Waislamu chini ya bendera ya tawhid na kuwaunganisha katika dola moja ambapo chini ya kivuli chake wanaishi maisha ya ukakamavu na heshima na kutokana nayo wanawashinda maadui, wanawanyenyekesha, kuwatawala na kuwaongoza kwa hukumu za uadilifu za Mwenyezi Mungu.

Uongozi wa kweli ni ule unaoweka ahadi yake kwa Mwenyezi Mungu juu ya vitendo vyake, kwa sababu unaamini kuwa huu ni wajibu juu yake na dhima ya kisheria ambayo lazima kushikamana nayo. Ni uongozi ambao unajadidisha ahadi hii kila leo na kuhakikisha kuwa hakuna mapumziko kwa ajili yake hadi sheria za Mwenyezi Mungu zitawale dunia na Uislamu uregeshe utukufu wake na kuwa ni uongozi pekee unaowaleta watu kutoka kwa kiza cha hukumu za mwanadamu kwenda katika mwangaza wa hukumu za Mola wa walimwengu, uongozi unaojali utekelezaji wa sheria za Mwenyezi Mungu na kuishi chini ya kivuli chake.

Ni uongozi uliounganishwa ndani ya chama cha kisiasa, Hizb ut Tahrir, ambacho kinafanya kazi kuregesha maisha kamili ya Uislamu, hakitaki wadhifa na hakitafuti heshima ya kidunia, bali kinamhofu Mwenyezi Mungu kana kwamba kinamuona na ni chenye uaminifu katika utekelezaji wa ahadi ilichoweka hadi bendera ya tawhid ipae angani na dini yote iwe kwa Mwenyezi Mungu pekee na hakuna amri ila Kwake. Ni uongozi mtukufu ulioje huu ambao ni mkweli kwa Mola wake: kwake Yeye unategemea, na katika ahadi Yake umekamata na kuwa na yakini.

**مِنَ الْمُؤْمِنِينَ رِجَالٌ صَدَقُوا مَا عَاهَدُوا اللَّهَ عَلَيْهِ فَمِنْهُم مَّن قَضَى نَحْبَهُ وَمِنْهُم مَّن يَنتَظِرُ وَمَا بَدَّلُوا تَبْدِيلاً**

**"Miongoni mwa Waumini wapo watu waliotimiza waioahidiana na Mwenyezi Mungu. Baadhi yao wamekwisha kufa, na baadhi wanangojea, wala hawakubadilisha (ahadi) hata kidogo."** [Al-Ahzab: 23].


Email: info@uqab.or.ke

# JIBU LA SWALI

## Amerika na Mabadiliko katika Mawakala wake nchini Pakistan



**Swali:**

Al Jazeera English iliripoti mnamo tarehe 28/04/2022 kwamba, “Waziri Mkuu wa Pakistan Shehbaz Sharif amemteua Bilawal Bhutto-Zardari, mtoto wa Waziri Mkuu wa zamani Benazir Bhutto, kama waziri wa mambo ya nje... Akiwa na umri wa miaka 33 tu, Bhutto-Zardari anakuwa mmoja wa mawaziri wa mambo ya nje wenye umri mdogo zaidi duniani... Sharif alitangaza baraza la mawaziri la watu 41 baada ya kuchukua nafasi ya waziri mkuu aliyeondolewa Imran Khan mapema mwezi huu......” Serikali ya Shebaz Sharif, ambaye alimrithi kaka yake Nawaz kama rais wa PML-N, aliapishwa mnamo tarehe 19/4/2022, yaani zaidi ya wiki moja baada ya kuondolewa kwa Imran Khan.

Swali ni nini kilisababisha mabadiliko haya? Kumbuka kuwa Bunge kwa kuungwa mkono na jeshi lilimpa imani Imran wakati anateuliwa, huku jeshi likiwa na hasira na pande mbili za PML-N na PPP wakati huo. Kwa hiyo nini kimetokea tangu hapo? Je, Marekani ina mchango katika suala hilo, ikijua kwamba imekuwa nyuma ya utawala wa Pakistan kwa miaka mingi?

**Jibu:**

Ili kufafanua majibu ya maswali haya, tunahakiki yafuatayo:

**Kwanza, Je, Imran Khan alifikiaje utawala?**

1- Jeshi ndilo lililompa Imran Khan madaraka. Imran Khan aliendesha serikali ambayo haikuwa na kifani kuhusiana na majenerali. Amelaumiwa kwa kuwa karibu sana na jeshi tangu alipoahidi kuunda "Pakistan Mpya," kuondoa ufisadi na upendeleo, baada ya kushinda uchaguzi wa 2018. Hadi hivi majuzi, Imran Khan alielezewa kama mmoja wa washirika wa karibu wa jeshi la Pakistan, kati ya wakuu wa serikali. Imran alishutumiwa hata kuwa chini ya jeshi.

Lau isingekuwa msaada wa jeshi kwake, Imran Khan asingepata imani yoyote ya kutawala! Mnamo 1996, alitangaza kuunda chama chake cha kisiasa cha Pakistan Tehreek e Insaf (PTI). Mnamo 1997, Imran Khan alishindwa kushinda hata kiti kimoja katika Bunge la Kitaifa wakati wa uchaguzi mkuu. Ilikuwa ni mwaka wa 2013 tu ambapo chama chake kiliweza kuleta athari katika siasa za Pakistan, kutokana na kuungwa mkono na Jeshi la Pakistan. Chama chake kilifanikiwa kushinda viti 30 katika Bunge la Kitaifa. Kilikuwa chama cha tatu kwa ukubwa cha upinzani, baada ya Pakistan Muslim League-Nawaz na Pakistan People's Party. Jeshi lilichagua kumpa Khan nafasi ya kushinda uchaguzi wa 2018. Hata hivyo, hiyo ilikuwa ni baada ya Imran Khan kukubaliana na Mkuu wa Majeshi, Qamar Bajwa, kuendesha uchaguzi mkuu.

2- Jeshi, pamoja na ujasusi chini ya uongozi wa Luteni Jenerali Faiz Hameed, walifanya kazi bila kuchoka kuboresha matarajio ya kisiasa ya Khan. ISI ilisaidia kupanga mikusanyiko yake kote nchini, na kumfanya kuwa mgombea aliyeshinda. Huku wakitishia wanahabari kuhusu kutoa utangazaji mzuri wa PML-N, huduma za usalama zilishambulia PML-N, kuwakamata, kuwaweka kizuizini na kuwanyanyasa wafanyakazi wa PML-N - mrengo wa Nawaz. Wanajeshi pia walifanya kazi nyuma ya pazia kuwanyima wagombea wa PML-N kugombea...

3- Ingawa chama cha Imran Khan kilishinda viti 149 katika Bunge la Kitaifa, bado kilikuwa chini ya viti 172 vinavyohitajika kuunda serikali ya wengi. Walakini, iliweza kufanya hivyo katika mfumo wa serikali ya mseto, kwa mpangilio wa jeshi. Serikali ya mseto ilikuwa ni mpango wa Jeshi la Pakistan kuhakikisha kuna njia ya kurudi nyuma, ikiwa Imran Khan atabadilisha mawazo yake na kuchukua hatua dhidi ya jeshi. Ujasusi pia ulifanikiwa kuwashawishi wanachama wa Pakistan People's Party katika serikali ya Imran Khan. Kwa hivyo, jumla ya wanachama 17 wa timu ya Imran Khan waliteuliwa chini ya ushawishi wa ISI. Ni wajumbe watatu pekee wa baraza la mawaziri ndio waliokuwa wafuasi wa PTI ambao hawakuwahi kuwa katika chama chengine chochote hapo awali!

***Endelea... UK 10***


Email: info@uqab.or.ke

**Pili: Baada ya Imran Khan kuwa Waziri Mkuu, alitoa huduma nyingi kwa Amerika,**

1- Idhaa ya TV ya Geo News ya Pakistan iliripoti kuhusiana na Khan kwamba, "Alipokea barua kutoka kwa Rais Trump wa Marekani mapema leo 3/12/2018, ambapo aliiomba Pakistan kuchukua nafasi katika mazungumzo ya amani ya Afghanistan na kusaidia kuleta harakati ya Taliban katika meza ya mazungumzo," kama ilivyoripotiwa kimataifa na Sputnik ya Urusi mnamo tarehe 3/12/2018. Kisha Imran Khan alikutana siku mbili baadaye na Mjumbe Maalum wa Marekani Khalilzad mjini Islamabad, akithibitisha maendeleo ya Pakistan kuhusiana na mpango wa Marekani kwa Afghanistan!

2- Waziri wa zamani wa Ulinzi wa Pakistan, Khawaja Asif, alithibitisha usaliti wa watawala wa Pakistan, wakati yeye ni mmoja wao. Katika mfululizo wa nukuu za tweets, Khwaja Asif alisema mnamo 3/1/2018, "Umeuliza tulifanya nini? Dikteta amesalimu amri kwa simu moja, nchi yetu ilishuhudia umwagaji damu mbaya zaidi, ulifanya mashambulizi 57,800 dhidi ya Afghanistan kutoka kwa vituo vyetu, majeshi yako yalipewa silaha na vilipuzi kupitia ardhi yetu, maelfu ya raia na askari wetu wakawa wahanga wa vita vilivyoanzishwa na wewe... Tulimwona adui yako kuwa ni wetu, tuliijaza Ghuba ya Guantanamo, tulikutumikia kwa shauku kubwa kiasi kwamba tuliiacha nchi yetu na shehena ya mizigo na uhaba wa gesi. Tulijaribu kukufurahisha kwa gharama ya uchumi wetu, tulitoa makumi ya maelfu ya visa kama matokeo ambayo mitandao ya Black Water ilienea katika nchi yetu. Hakuna jambo lililo wazi zaidi kuliko hili: Pakistan ilipigana vita ambavyo havikuwa vita vyake... Ilimwaga damu ya watoto wa Kiislamu kwa ajili ya Marekani... Na ilifuja maadili ya Dini yake ya Kiislamu, ili kutumikia maslahi ya Marekani…

3- Kadhalika kuhusu India, kama alivyoshindwa hapo awali, Imran alinyamaza kuhusu unyakuzi wa India wa Kashmir, isipokuwa kwa misimamo ya kupiga domo tupu. Kwa hivyo tulisema katika swali na jibu la 8/8/2019, "Wakati India ilipotangaza uamuzi wake wa hivi karibuni wa kubatilisha hadhi maalum ya Kashmir, msimamo wa Pakistan pia ulikuwa wa kuvunja moyo, haukupita zaidi ya kulaaniwa pekee, ili kuondoa lawama. Wizara ya Mambo ya Nje ya Pakistan ilitoa taarifa ikisema, 'Pakistan inalaani vikali na kukataa matangazo yaliyotolewa leo (Jumatatu 5/8/2019) na New Delhi. Hakuna hatua ya upande mmoja ya Serikali ya India inayoweza kubadilisha hali hii yenye mzozo, kama ilivyoainishwa katika maazimio ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa (UNSC), Pakistan itatumia machaguo yote yanayowezekana ili kukabiliana na hatua hizo zisizo halali.' (AFP 5/8/2019)... Kwa maana nyengine, mithili ya Mamlaka [ya Palestina] ya Abbas na nchi za Kiarabu zinazowazunguka, wanashutumu na kupinga ukiukaji wa umbile la Kiyahudi wa Ardhi Tukufu ya Palestina bila kuhamasisha majeshi kupigana. Pakistan inarudia dori lile lile na kushutumu bila ya kuhamisha jeshi kupigana! [Mwisho wa Nukuu]

4- Imran Khan aliamiliana na Mfuko wa Fedha wa Kimataifa (IMF), wakati mfuko huu uko chini ya udhibiti wa Marekani. Imran Khan alitekeleza sera zake, baada ya kuzungumza dhidi ya kukabiliana na IMF katika kampeni yake ya kuwania madaraka. Hakika, Imran alikuwa amesema kabla ya kuingia madarakani, katika mahojiano yaliyochapishwa katika gazeti la Uingereza, 'The Guardian,' mnamo tarehe 18 Septemba 2011, kwamba, "Nchi inayotegemea misaada? Mauti ni bora kuliko hayo. Inakuzuia kufikia uwezo wako, kama ukoloni ulivyofanya. Msaada ni udhalilishaji. Kila nchi ninayoijua ambayo imekuwa na mipango ya IMF au Benki ya Dunia imefukarisha tu maskini na kuwatajirisha matajiri." Hata hivyo, alipoingia madarakani alikanusha ahadi yake! Mazungumzo na Mfuko wa Fedha wa Kimataifa yalianza kwa dhati. Kisha, mnamo tarehe 3 Julai, 2019, Mfuko wa Fedha wa Kimataifa (IMF) ulikubali kupanga mkopo wa dolari bilioni 6 kwa Pakistan chini ya Mpango wa Hazina ya Muda wa Miezi 39 (EFF)...

5- Waziri Mkuu wa Pakistan, Imran Khan, alikumbuka huduma kwa Amerika, katika mahojiano na Fox News mnamo Jumatatu 22/7/2019, akisema, "Sisi Pakistan kila wakati tulihisi kuwa sisi ni mshirika wa Amerika na ikiwa tulikuwa tumepewa taarifa kuhusu Osama bin Laden, tulipaswa kumtoa nje. Na bado ISI ndiyo iliyotoa taarifa iliyopelekea kulitambua eneo aliko Osama bin Laden. Ukiiuliza CIA ilikuwa ni ISI ndiyo iliyotoa eneo la awali kupitia unganisho la simu." Alisema hayo "katika ziara ya kwanza ya shujaa wa zamani wa kriketi katika Ikulu ya White House, tangu kuchaguliwa kwake mwaka mmoja uliopita nchini Pakistan, ambapo alikutana na Rais wa Marekani Donald Trump," kama ilivyoripotiwa na Al-Quds Al-Arabi mnamo 23/07/ 2019.

**Tatu: Uhusiano wenye mvutano kati ya Imran na uongozi wa jeshi, na kisha Marekani:**

Imran Khan aliendelea kuwa chini ya udhibiti wa jeshi, na Marekani nyuma yake, kwa takriban miaka mitatu ya utawala wake. Mwishoni mwa mwaka wa tatu, uhusiano wake na Mkuu wa Jeshi Bajwa ulizidi kuwa mbaya, kama ilivyokuwa baadaye na Amerika kwa kuunga mkono msimamo wa jeshi. Imran alikataa kumkubali mgombea wa jeshi kwa nafasi ya mkuu wa ISI. Luteni Jenerali Anjum Nadeem aliposimamishwa katika uteuzi huo, jambo ambalo lilisababisha hali ya wasiwasi katika jeshi... Kama ilivyoripotiwa na tovuti ya Al-Manar TV mnamo tarehe 27/10/2021, "Anjum atachukua wadhifa wake mpya mnamo tarehe 20 Novemba. Mnamo tarehe 6 Oktoba, Bajwa alimteua Anjum kuchukua nafasi ya mkuu wa ISI, Luteni Jenerali Faiz Hameed. Anjum alikuwa akichukua nafasi ya Kamanda wa Kikosi katika mji wa bandari wa kusini wa Karachi. Bajwa alimteua Hameed kama Kamanda wa Kikosi huko Peshawar mwezi huu. Imran Khan amekuwa akitangaza hadharani

*Endelea... UK 11*

kumuunga mkono Faiz Hameed kama kiongozi wa ujasusi wa ndani. Kwa hivyo, uhusiano wa serikali ya Imran Khan na jeshi uliharibiwa na mivutano, kufuatia kuteuliwa kwa Nadeem Anjum mahali pa Faiz Hameed. Hii ilikuwa hasa miongoni mwa uvumi ulioenea kwamba Khan angemteua Hameed kuchukua nafasi ya Qamar Javed Bajwa, ambaye muhula wake wa pili madarakani unamalizika Novemba 2022.

Kwa kweli, Amerika inasimama nyuma ya mkuu wa jeshi. Kwa hivyo, uamuzi ulifanywa ili kuandaa njia ya kuondolewa kwa imani kutoka kwa Imran Khan, sambamba na kutafuta mbadala wake. Imran Khan alipokea baadhi ya taarifa hizi. Kwa hiyo, Imran alijaribu kufanya upatanishi na uongozi wa jeshi. Alikubali kumteua Nadeem Anjum mahali pa rafiki wa Imran, Faiz Hameed. Hata hivyo, uongozi wa jeshi ulisisitiza, kwa msaada wa Marekani, kwamba Imran lazima aondolewe katika nafasi ya uwaziri mkuu, kwa kuteuliwa mtu mwingine! Jeshi na Amerika ziliogopa kwamba ukiukaji huu wa uamuzi wa jeshi ungesababisha kudhoofisha maamuzi ya jeshi, linaloungwa mkono na Amerika. Hivyo msisitizo wa kumuondoa Imran...

**Nne:** Imran Khan alifazaika, haswa kwa vile alitoa huduma kubwa kwa Amerika kama tulivyotaja, wakati vivyo hivyo, alitii uongozi wa jeshi ... ni kana kwamba aliamuru kwamba jeshi na Amerika zitafanya kazi ya kumtenga, baada ya huduma alizowapa. Hata hivyo, alisahau au kujisahaulisha kwamba nchi za makafiri haziruhusu mawakala wao kupata nafasi ya kupumua! Kwa vyovyote vile, alikasirishwa na jambo hili na akatoa kauli kuhusu Amerika, lakini wakati huo alikuwa amechelewa! Miongoni mwa kauli zake:

1- Kama ilivyoripotiwa na Euro News Arabia mnamo 4/2/2022, "Waziri Mkuu wa Pakistan Imran Khan aliambia kundi la waandishi wa habari wa kigeni leo, Jumamosi, 'Hatua ya kuniondoa ni kuingiliwa kwa wazi kwa siasa za ndani na Marekani." Gazeti la Arab Post la tarehe 3/4/2022 lilisema kuwa, "vyombo vya habari vya ndani viliripoti kwamba Khan alipokea ujumbe kutoka kwa balozi wa Islamabad jijini Washington ambao ulijumuisha rekodi ambayo afisa mmoja wa ngazi ya juu wa Marekani, anayesemekana kuwa Msaidizi wa Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani kwa Masuala ya Kusini na Kati ya Asia, Donald Lu, akitangaza kwamba Amerika ilihisi kuwa uhusiano unaweza kuwa bora ikiwa Khan ataondoka.

2- Katika hali inayotofautiana na msimamo wa Washington kuhusu Urusi kuhusiana na shambulizi lake dhidi ya Ukraine, Imran Khan alikataa kulaani shambulizi hilo na hata alitembelea Moscow, akitokea karibu na Rais wa Urusi Vladimir Putin, mnamo tarehe 24/2/2022, yaani siku ya kwanza ya vita vya Urusi dhidi ya Ukraine. Hii ni wakati ambapo mkuu wa jeshi la Pakistan, Qamar Bajwa, alilaani shambulizi hilo kwa uwazi, akiunga mkono msimamo wa Marekani na kupinga kauli za hivi karibuni za Khan. Al Hurra iliripoti mnamo 2/4/2022 kwamba, "mkuu wa jeshi la Pakistan alikosoa vita vya Urusi dhidi ya Ukraine, akitaka kusitishwa mara moja kwa kile alichoelezea kama "janga kubwa," lililoathiri nchi ndogo. Ni vyema kutambua kwamba ukosoaji wa Jenerali Qamar Javed Bajwa dhidi ya Moscow unakinzana na Waziri Mkuu wa nchi yake, Imran Khan. Imran Khan alitetea haja ya kutoegemea upande wowote kwa Islamabad, akiielekeza kwenye kile kinachotokea nchini Ukraine. Pia alikataa kukosoa vitendo vya Rais wa Urusi Vladimir Putin.

3- Katika hali nyingine, kama ilivyoripotiwa na 'The New Arab,' mnamo tarehe 7/3/2022, "Imran Khan alizungumza kuhusu mabalozi wa Muungano wa Ulaya kuandika barua ya kumtaka alaani operesheni ya kijeshi ya Urusi nchini Ukraine... Imran alisema. , ‘Nataka kuwauliza mabalozi wa Muungano wa Ulaya: Je, mliiandikia India barua kama hiyo?’ Akaongeza, ‘Mnaonaje kutuhusu? Je, sisi ni watumwa wenu...kwamba chochote mtakachosema, tutafanya?’ Mpakistani huyo aliamua kuendelea, “Wakati India ilipokiuka sheria za kimataifa huko Kashmir na Maazimio ya Baraza la Usalama la Marekani, je, yeyote kati yenu [mabalozi wa EU] aliikosoa India. Je, mulivunja uhusiano na India? Au kusimamisha biashara nao?”

**Tano:** Kama tulivyosema hapo juu, Imran Khan hakutarajia kwamba utumishi wake wote kwa jeshi, na nyuma yake, Amerika, haungekuwa na manufaa kwake! Ni kana kwamba hakutambua kwamba yeyote anayeingia madarakani kwa kuungwa mkono na makafiri wa kikoloni, kama wakala wao, anakuwa kama kipande cha chesi kwao. Wanamwendesha wapendavyo. Zaidi ya hayo, wanamtoa kama wapendavyo, bila kusita, ikiwa hatafikia masilahi yao. Hiki ndicho kilichotokea kwa Imran Khan! Mnamo tarehe 7/4/2022, uamuzi wa Naibu Spika ulikataa kura ya hoja ya upinzani ya kutokuwa na imani dhidi ya serikali ya Imran Khan. Pia ulibatilisha uamuzi wa Rais wa Jamhuri wa kulivunja Bunge tarehe 3/4/2022 na kuelekea kwenye uchaguzi wa mapema, kwa ushauri wa Waziri Mkuu Imran Khan. Mahakama iliamua kuwa hatua hii ni kinyume na katiba na hivyo kuwa batili. Mahakama kuu pia ilimuamuru spika wa bunge kufanya kikao cha Bunge tarehe 10/4/2022, ambapo Bunge la Pakistan lenye viti 342 lilipiga kura 174 za kutokuwa na imani na Imran Khan... Ni wazi kuwa katika matukio haya, jeshi lilikuwa likiendesha mambo nyuma ya pazia. Majaji wakuu hawangeweza kamwe kuchukua uamuzi kama huo bila kuungwa mkono kikamilifu na mkuu wa jeshi...

**Sita:** Siku iliyofuata, 11/4/2022, Bunge lilimchagua Shehbaz Sharif kuwa Waziri Mkuu, hadi tarehe ya uchaguzi mkuu wa Agosti 2023. Kuhusu Shehbaz, yeye ni kaka mdogo wa Nawaz Sharif, ambaye alikuwa wa kwanza. Waziri Mkuu wa Pakistan. Shehbaz amekuwa kiongozi wa upinzani katika Bunge la Pakistan tangu 2018. Shehbaz alichukua uongozi wa Pakistan

***Endelea... UK 12***

Muslim League baada ya kaka yake Nawaz, ambaye alianzisha chama. Shehbaz alijitolea kuwa mtiifu kwa jeshi na Marekani... na kisha jeshi likamuunga mkono katika uchaguzi wa kuchukua nafasi ya Imran Khan na akafanya yafuatayo:

1- Shehbaz alianza muhula wake wa kisiasa kulingana na Amerika inavyotaka... Alianza kwa sauti ya maridhiano na India, akisema kuwa yuko tayari kwa mazungumzo badala ya makabiliano. Sky News kwa Kiarabu iliripoti mnamo 14/4/2022 kwamba "Katika hotuba yake ya kwanza, Shehbaz Sharif alisema, 'Tunataka uhusiano mzuri na India lakini hakuwezi kuwa na amani endelevu isipokuwa suala la Kashmir litatuliwe,' huku akitoa wito kwa Waziri Mkuu wa India kuruhusu utatuzi wa suala la Kashmir na hivyo nguvu zitolewe kwa ajili ya ustawi wa nchi hizo mbili. Waziri Mkuu wa India Modi alimjibu kwa kutuma barua pepe, "Hongera H.E. Mian Muhammad Shehbaz Sharif kwa kuchaguliwa kwake kama Waziri Mkuu wa Pakistan. India inatamani amani na utulivu katika eneo lisilo na ugaidi, ili tuweze kuzingatia changamoto zetu za maendeleo na kuhakikisha ustawi wa watu wetu. Kumbuka kuwa Waziri Mkuu wa India anachukia Uislamu na Waislamu. Modi anawachochea wafuasi wake wa Kibaniani dhidi ya Waislamu nchini India. Wafuasi wake wanawawekea vikwazo Waislamu na hawakubali Waislamu waishi katika nchi yao ya India. Wanawawekea vikwazo mabinti wa Kiislamu shuleni katika suala la kanuni za mavazi ya Kiislamu.

2- Ripoti za habari zinataja kwamba Shehbaz Sharif alijitolea kufanya kazi na majenerali, ikiwa atachaguliwa. Alisema nchi hiyo ilihitaji kusonga mbele na kuondokana na tofauti na jeshi. Hapo awali alikuwa amelikosoa jeshi katika mapinduzi yake dhidi ya kaka yake mkubwa, Waziri Mkuu wa zamani, Nawaz Sharif, mwaka wa 1999. Shehbaz Sharif alishiriki katika uchaguzi wa 2018 lakini alishindwa na Imran Khan. Mnamo Disemba 2019, Afisi ya Kitaifa ya Uwajibikaji ilizuia mali 23 zinazomilikiwa na Shehbaz na mwanawe, na kuwashtaki kwa ulanguzi wa pesa. Mnamo Septemba 2020, Shehbaz alikamatwa kwa tuhma za kuhusika na ulanguzi wa pesa, lakini aliachiliwa mnamo Aprili 2021 kwa dhamana. Kwa hivyo, maridhiano yake na jeshi ilikuwa moja ya sababu zilizomruhusu kushika madaraka.

3- Hebu turegelee hapa pongezi za haraka za Amerika kwa Shehbaz Sharif, kama Waziri wake wa Mambo ya Nje, Blinken, alisema, "Marekani inampongeza Waziri Mkuu mpya wa Pakistan Shehbaz Sharif na tunatarajia kuendeleza ushirikiano wetu wa muda mrefu na serikali ya Pakistan...” (Sky News 4/14/2022). Hii inathibitisha kwamba Marekani imekubali maridhiano ya Shehbaz na jeshi, pamoja na ahadi yake ya kutekeleza sera ya Marekani. Ilikubali kupanga mafanikio yake ya kuingia madarakani, baada ya kuwazuia yeye na kaka yake Nawaz hapo awali. Sasa Marekani imekubali tu baada ya Shehbaz kuwa tayari kabisa kufanya kazi na Marekani, wakati yeye ameshapatana na jeshi ambalo ni tiifu kwa Marekani!

4- Sauti ya Amerika (VOA) iliripoti mnamo tarehe 12/4/2022, kwamba "serikali mpya ya Pakistan ilisema Jumanne "itazungumza kwa njia ya kujenga na chanya" na Marekani ili kukuza "malengo ya pamoja" ya amani ya kikanda, usalama na maendeleo... "Tunakaribisha uthibitisho wa Marekani wa uhusiano wa muda mrefu na Pakistan," afisi ya Sharif ilisema katika kujibu matamshi ya mwandishi wa habari wa White House Jen Psaki siku ya Jumatatu ambapo alisisitiza ukosoaji wa uhusiano wa Washington na Islamabad bila kujali kiongozi wake. "Tunatazamia kuimarisha uhusiano huu muhimu juu ya kanuni za usawa, maslahi ya pande zote na manufaa ya pande zote," taarifa ya Pakistan ilisema. Siku ya Jumatatu, Psaki alisema utawala wa Biden unaunga mkono "kudumishwa kwa amani kwa kanuni za kidemokrasia za kikatiba" na hauungi mkono chama kimoja cha kisiasa dhidi ya kingine nchini Pakistan. "Tunathamini ushirikiano wetu wa muda mrefu na Pakistan, siku zote tumeiona Pakistan yenye ustawi na ya kidemokrasia kama muhimu kwa maslahi ya Marekani," alisema. Psaki alisema uhusiano "wa muda mrefu, wenye nguvu na wa kudumu" utaendelea chini ya viongozi wapya jijini Islamabad."

Hii inathibitisha kwamba Amerika ilikuwa nyuma ya anguko la wakala wake wa zamani, Imran Khan, na kupandishwa cheo kwa Shehbaz Sharif, ambaye anatangaza waziwazi nia yake ya kufanya kazi na Marekani, kwa nguvu zaidi kuliko Imran Khan alivyofanya!

**Saba:** Mawakala hawa hawajifunzi wala hawafikirii. Iwapo Marekani itampindua mmoja wao, wanakimbilia kusuhubiana na Marekani na kujiandaa kutoa huduma kwa Amerika, hadi wafikie kutawala. Inawafafanua kuwa ni duni kuliko viongozi halisi wa kisiasa wa kimfumo, wanaotafuta nyadhifa pekee. Shehbaz Sharif hakujifunza kutoka kwa Amerika kumpindua kaka yake zaidi ya mara moja, wakati yeye pamoja naye waliadhibiwa kwa kupelekwa uhamishoni. Ummah unahitaji wanasiasa wenye maadili wanaoshikamana na mfumo, ambao ni mfumo wa Umma, Uislamu. Uislamu pekee ndio unaoyachukulia mambo yote kwa njia kimsingi na sahihi, huku wanasiasa wake pekee ndio wanaoweza kuuokoa Ummah, kuuhuisha na kuufanya kuwa na dola kuu, sio nchi inayonyenyekeshwa chini ya Amerika.

Kwa hakika, Pakistan inastahiki kuwa nukta ya nusra kwa dola hii tukufu, dola ya Khilafah Rashida, kwa idhini ya Mwenyezi Mungu (swt).

**إِنَّ فِي هَذَا لَبَلَاغاً لِقَوْمٍ عَابِدِينَ**

**“Hakika katika haya yapo mawaidha kwa watu wafanyao ibada.” [Sura Al-Anbiyyah 21:106]**

**5 Shawwal 1443 H**
**5/5/2022 M**



Email: info@uqab.or.ke